# Kutoka Mgogoro hadi Mazungumzo

**Je, masaibu yanakunyang'anya furaha, nguvu, ama tija?**

**Je, masaibu yako yapo nyumbani, kazini, au katika kitongoji chako?**

**Je,hauwezi kumpata jirani, mwanafamilia, msimamizi wako, au mfanyakazi mwenza asikilize mahangaiko ama hisia zako?**

**Unataka kukomesha mgogoro sumbufu, au unahitaji njia mbadala isiyohusisha sheria.**

Wataalamu wa kuingilia kati mgogoro husaidia watu kuzungumza kuhusu masaibu ambayo husababisha mafadhaiko, hasira na kukata tamaa. Ni kuhusu kudhihirisha mitazamo, hisia, na uzoefu. Upatanisho ni njia iliyothibitishwa vyema na maarufu kwa kukabiliana na mgogoro.



# Je, Kuingilia kati Mgogoro ni nini?

Kuingilia kati mgogoro ni njia ya watu kuzungumzia masuala magumu kati yao ambayo husababisha mafadhaiko, hasira na kukata tamaa. Husaidia watu kutambua wasiwasi na masaibu kwa njia inayofaa, na kuwafanya wawe na maoni mazuri zaidi yenye kupanua ufahamu. Hii husaidia watu waamue vizuri zaidi wanayopaswa kufanya kuhusu hali yao.

Wapatanishi hutegemeza haya mazungumzo magumu kwa kuwasaidia watu kujadili na kila mmoja vyema zaidi ili mazungumzo yasiharibike zaidi.

Wataalamu wetu wa kuingilia kati mzozo huzungumza na washiriki kabla ya kikao cha kuingilia kati ili wawasaidie kujitayarisha. Watu wanaofikiria hatua kama vile upatanisho wanaweza kufikiria kuhusu wasiwasi, mahitaji na chaguzi mbalimbali ambazo zaweza kusaidia kushughulikia hali hiyo vizuri zaidi.

**Kuzungumza kuhusu uwezekano wa kutumia huduma za upatanisho au huduma nyingine za kuingilia kati mzozo, piga simu kiurahisi katika kituo cha Upatanisho cha Dayton kwa 937.333.2345. Msimamizi wa kesi atasikiliza wasiwasi wako na atajibu maswali yako kusudi akusaidie kuamua juu ya huduma zetu.**





# Ni nani wanaofaidika na Huduma Zetu?

Huduma za Upatanisho za Kituo cha Dayton zinaweza kufikiwa na mtu yeyote. Nafasi za kuelekeza wengine pia zipo kwa washiriki wa jamii kama vile mashirika ya huduma za jamii, waajiri wa umma na wakibinafsi, majirani na familia.

**Watu binafsi na vikundi vinavyonufaika moja kwa moja :**

- Watu binafsi wakiwemo wanakaya, marafiki, majirani
- Wazazi wakiamua mipango ya ziara
- Wasimamizi wa majengo na wapangaji
- Familia zinapofanya uamuzi wa kutunza au mambo mengine
- Wafanyikazi na wasimamizi
- Mashirika
- Makampuni na biashara
- Shule za umma na za kibinafsi, vyuo vikuu na vyuo vya kati
- Mashirika ya kutekeleza sheria
- Mifumo ya mahakama

# Kituo cha upatanisho cha Dayton

Kituo cha Upatanisho cha Dayton ni shirika la wataalamu tajika wa kuingilia migogoro na watu wakujitolea katika jamii ambao hutoa huduma kwa wale wanaokabiliwa migogoro. Kituo kimeibuka kuwa cha kutegemewa kwa kuboresha hali ya maisha katika Dayton na kusaidia watu binafsi, familia, na mashirika kubadilisha mgogoro uwe mazungumzo. Huduma ni bure kwa wakaaji wa Dayton na zinapatikana kwa mashirika au wale wanaoishi nje ya Dayton kwa bei nafuu.

Kituo husaidia kukabiliana na migogoro kabla haijakuwa mbaya zaidi. Tunasaidia watu kuepuka mambo hasi na haribifu ya kuwa katika mgogoro. Wataalamu wetu wa kuingilia mgogoro husaidia washiriki kushughulikia hali yao. Hii inaweza kusaidia kupunguza kutoelewana na kuboresha mawasiliano.

Kituo hutoa huduma mbalimbali za kuingilia kati migogoro ili kusaidia kutatua mgogoro kabla, wakati wa au baada ya unapofanyika. Kituo pia kinatoa mafunzo – “Kukabiliana Inavyofaa na Mgogoro” – kwa watu binafsi na mashirika wanaotaka kujifunza ujuzi wa kuingilia kati mgogoro vyema.

*“Nilihisi kwamba wapatanishi walifanya kazi nzuri sana ili kusaidia kutatua suala hilo!”*

*Mshiriki wa Upatanisho*

Dayton Mediation Center
from conflict to conversation

## Nini Hutendeka katika kikao cha Kuingilia kati?

Upatanisho ni mazoezi ya kuheshimiwa kutokana na ukale wake ambao unaweza kusaidia watu wenye hali mbalimbali ngumu. Huduma mbalimbali za kuingilia kati mgogoro katika Kituo cha Upatanisho cha Dayton husaidia watu kudhihirisha mitazamo, hisia na uzoefu ili waweze kusonga mbele inavyofaa wakishughulikia hali yao.



Katika mazingira ya siri, wataalamu wetu wa kuingilia mgogoro husaidia washiriki kufikiria na kuzungumza kuhusu mgogoro kwa ukamilifu zaidi. Kwa sababu hiyo, watu wanaweza fanya mabadiliko makubwa katika kuelewa kwao ili kuwasaidia vyema zaidi na kwa uhakika zaidi waweze kuzungumzia yaliyo muhimu kwao kuhusu hali zao. Huu ndio mwanzo wa kusonga kutoka mgogoro hadi mazungumzo.

Washiriki husaidia kubuni na kutengeneza harakati zao wenyewe za kuzungumza na kufanya maamuzi. Wataalamu wetu wa kuingilia kati mgogoro watasaidia watu kwa kusikiliza kwa umakini washiriki wanapozungumzia hali hio. Wataalamu wataingilia kati, inapohitajika, ili kuwasaidia watu waelewe habari na kuelekeza maamuzi kuhusu wanayopaswa kufanya Kamwe hawafai kutawala kikao, kusuluhisha tatizo ama kutumia mamlaka.

## Mgogoro ni nini?

Mgogoro ni kipeo cha tatizo kwa njia tunayoingiliana wenyewe. Inakuwa vigumu kuongea, kusikiliza, na kusikia mitazamo. Hata tunapofanya yote tuwezayo kushughulikia masuala, bado yanaweza baki. Mgogoro ni tukio la kawaida katika maisha. Tunaweza kufaidika kwa kutafuta msaada wakati ambao sisi wenyewe tumeshindwa kuyaelewa mambo.

**Je, Mgogoro Hukabiliwa vipi?**

Hakuna apendaye mgogoro lakini mara nyingi kutatua tatizo, watu wanapaswa kulipitia. Mara tu watu wanapokuwa katika mzozo, changamoto ni: je, unatatuliwa vipi?

Jambo muhimu ni kuunganisha watu na nyenzo vya kuingilia kati kabla mgogoro haujakuwa mharibifu na wakudhuru. Kituo cha Upatanisho cha Dayton ni chaguo nzuri kwa kusuluhisha mgogoro. Tunaweza kukupatia njia ya kupata suluhisho linalowezekana ambalo hutahusisha mfumo wa mahakama ama kutumia rasilmali chache isivyofaa.

*"Kukabiliana Inavyofaa na Mgogoro" lilikua la kubadilisha maisha kwangu. Kama "muepukaji mzozo" wa maisha, kabla ya darasa hilo, nilikuwa nafanya jitihada kuepuka kabisa mgogoro wowote. Baada ya kuhudhuria,siepuki tena mgogoro unaoweza kutokea na nimejua jinsi mgogoro ulivyo, wakati mwingine, unahitajika na unaweza kuwa uzoefu mzuri na wakufaidi. Hususani, nilijua jinsi ya kutambua waziwazi kile ninaweza kuthibiti na kile sina uwezo wa kudhibiti katika hali fulani.*

*Mfumo wa mgogoro ulioanzishwa unaweza saidia sana na unafafanua chaguzi za kujibu pamoja na matokeo ya chaguzi zilizoteuliwa. Ingawa nilikazia fikira kwa mgogoro, pia kwa halisi niliimarisha stadi zangu za mawasiliano na kusikiliza.*

*Laura*

## Kuhudumia Jamii ya Dayton na Hata mbali zaidi

Kituo cha Upatanisho cha Dayton kilianzishwa mwaka wa 1987 katika jitihada za kupunguza athari za migogoro ya jamii kwa mali ya umma. Tangu wakati huo, wanajamii kotekote katika eneo hilo wameshauriana na Kituo kwa mwongozo wa kuchagua huduma ya kuingilia mgogoro inayofaa ikiwemo:

- Upatanisho
- Maelekezo kuhusu migogoro
- Mafunzo
- Kuwezesha
- Ushirikiano wa Kikoa

Mapendekezo kwa ajili ya huduma kutoka Kituo cha Upatanisho cha Dayton yanaweza kufanywa na watu binafsi, mashirika ya huduma za jamii, mifumo ya mahakama, mashirika ya kutekeleza sheria, na mashirika. Kutumia huduma zetu za kuingilia mgogoro ni hatua yenye mwelekeo sahihi wa kubadilisha mgogoro kuwa mazungumzo. Wacha tushauriane na wewe na tukuelekeze kwa njia hakika ya kusonga mbele.

**Jihusishe!**

Kituo kina nafasi mbalimbali za kujitolea kwa wanajamii wanaopendelea:

- Wapatanishi
- Wanajopo wa Athari za Jamii
- Wapokea-wageni Jumamosi
- Mwanachama wa Bodi ya Ushauri
- Watafsiri wa Lugha
- Mchango

**Ukitaka kujitolea jaza ombi la kujitolea kwa:**
**www.daytonmediationcenter.org**

**NAFCM**
**Mwanachama**

**ISCT**
**Tawi la shirika**

Dayton Mediation Center
from conflict to conversation


371 West Second St.
Ghorofa la 3
Dayton, Ohio 45402

937-333-2345

**daytonmediationcenter.org**